# Kusiluka ataka Tehama isiharibu usalama, umoja

**Na Selemani Nzaro, Arusha**

KATIBU Mkuu Kiongozi, Balozi Dk Moses Kusiluka amesema matumizi mabaya ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yanachangia kuvuruga usalama wa nchi, umoja na mshikamano wa taifa na kutoa mwanya kwa uhalifu wa kimtandao.

Balozi Dk Kusiluka alisema hayo wakati akifungua kikaokazi cha sita cha Serikali Mtandao kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC) jijini Arusha jana.

Alisema kutokana na uwepo wa changamoto ya usalama wa kimtandao, matumizi ya teknolojia zinazochipukia ikiwemo akili unde, kikao kitakuja na maazimio ya namna ya kutumia teknolojia hizo kwa uadilifu ili kulinda maslahi, mila na desturi za taifa.

Balozi Dk Kusiluka aliridhishwa na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Serikali Mtandao, ikiwemo ni pamoja na kuimarika kwa usimamizi wa miradi ya Tehama serikalini. Alisema mafanikio mengine ni uendeshaji wa Mtandao wa Mawasiliano wa Serikali (GOVNET) na uimarishaji na usimamizi wa vituo vya serikali vya kuhifadhi data, pamoja na kuwepo kwa mifumo shirikishi inayowezesha serikali kutekeleza majukumu yake.

Alisema jitihada hizo zimeiwezesha serikali kupunguza urudufu wa mifumo, kuwezesha ubadilishanaji wa taarifa baina ya taasisi za umma kupitia mifumo ya Tehama na kuongeza tija, ufanisi na uwajibikaji katika utendaji kazi wa serikali.

Balozi Dk Kusiluka alipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) kupitia kituo chake cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (eGOVRIDC) kwa juhudi za kuendeleza tafiti na bunifu za kidijiti, hasa katika teknolojia zinazoibukia.

"Serikali inatambua na kuthamini mchango wa sekta binafsi katika safari ya kujenga Serikali Mtandao. Ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi, zikiwemo benki, kampuni za mawasiliano na watoa huduma za Tehama, ni nguzo muhimu ya mafanikio ya mageuzi ya kidijitali," alisema.

Balozi Dk Kusiluka alisema mafanikio ya Tanzania kutambuliwa kimataifa kupitia tuzo za Umoja wa Mataifa (UN) na tathmini ya Benki ya Dunia ya Tanzania kufanya vizuri katika matumizi ya mifumo ya mawasiliano serikalini ni ushahidi kuwa nchi ipo katika mwelekeo sahihi wa mageuzi ya kidijiti serikalini.

Amezielekeza taasisi zote za umma zizingatie Sheria ya Serikali Mtandao ya mwaka 2019, kanuni zake, viwango na miongozo ya serikali mtandao kwa ukamilifu wake.

"Mnafahamu taratibu nzima zinazopaswa kufuatwa, ikiwa ni pamoja na kuwasilisha andiko la mradi e-GA kabla ya kuanzisha miradi hiyo. Nawaelekeza kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa. Wale wote watakaokaidi sheria hii watachukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria," alisema Balozi Dk Kusiluka.

Ameiagiza e-GA iwasilishe taarifa serikalini kuhusu miradi yote ya Tehama ambayo haikuzingatia sheria, kanuni na viwango vya Serikali Mtandao ili hatua zichukuliwe kwa wahusika kwa mujibu wa sheria.

# TMA yatabiri mvua kubwa mikoa minane

**Na Anna Mwikola**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imetabiri mvua kubwa zinatarajiwa kunyesha katika mikoa minane ndani ya siku tano, kuanzia Februari 16 hadi Februari 20.

Taarifa ya TMA iliyotolewa jana imetaja mikoa itakayoguswa na mvua hizo kuwa ni Dodoma, Morogoro, Rukwa, Iringa, Njombe, Songwe, Mbeya na Ruvuma.

TMA imeeleza kuwa mvua za kiwango cha wastani zinatarajiwa kunyesha katika mikoa hiyo kati ya jana na leo na athari zinazoweza kutokea ni baadhi ya makazi kuzungukwa na maji.

Mvua hizo ni nje ya mvua za msimu wa Masika zilizotabiriwa kuanza wiki ya mwisho ya Februari kwa baadhi ya mikoa na wiki ya kwanza na ya pili ya Machi kwa mikoa mingine inayopokea mvua hizo. Pia, ni nje ya mvua za msimu wa Vuli zilizoanza Novemba 2025 na zinazotarajiwa kumalizika Aprili 2026.

Mtaalamu wa hali ya hewa wa TMA, Alfred Kondowe aliliambia HabariLEO jana kuwa mikoa ya katikati mwa nchi, ikiwemo Dodoma na Singida pamoja na Nyanda za Juu Kusini Magharibi ambazo ni Songwe, Mbeya, Iringa na Njombe ilitarajiwa kuwa na vipindi vichache vya mvua kubwa.

Kondowe alisema leo mikoa ya Kagera, Mwanza, Simiyu, Geita, Mara na Shinyanga inatarajiwa kuwa na vipindi vichache vya mvua kubwa, pamoja na mikoa ya Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki ambayo ni Kilimanjaro, Arusha na Manyara.

Kondowe alisema sababu za mvua hizo ni kuimarika kwa baadhi ya mifumo ya hali ya hewa.

"Angalizo ambalo tumetoa ni kwa ajili ya wananchi kuchukua hatua stahiki kujikinga na madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na mvua hizi kubwa zilizotabiriwa katika maeneo hayo," alisema.

Aliongeza: "Hadi kufikia leo (jana) mchana, vituo vyetu vya hali ya hewa

# Wanawake na Samia, vijana walamba bilioni 2/- za CRDB

**Mwandishi Maalumu**

MBUNGE wa Mtumba na Waziri wa Madini, Anthony Mavunde ameipongeza Taasisi ya Benki ya CRDB kwa kutenga Sh bilioni mbili kuwezesha wanachama wa Umoja wa Wanawake na Samia na vikundi vya vijana mkoani Dodoma kupitia Programu ya iMbeju.

Uwezeshaji huo ulitangazwa jijini Dodoma jana katika semina iliyoandaliwa na taasisi hiyo ya CRDB kwa kushirikiana na Ofisi ya Mbunge wa Jimbo la Mtumba.

Katika hafla hiyo, Mavunde alikabidhi mfano wa hundi ya Sh bilioni mbili kwa wanawake na pikipiki 20 zilizotolewa kwa vikundi 10 vya vijana ili kuimarisha shughuli za kiuchumi.

Mavunde alisema uwezeshaji huo unaendana na juhudi za serikali za kuchochea ajira, kuongeza kipato cha kaya na kukuza biashara ndogo na za kati.

"Fedha hizi mlizotenga na mlizoanza kuzitoa leo (jana) ni muhimu sana kwa maisha ya wajasiriamali wetu. Ninaamini Wanawake na Samia watakuwa mfano bora wa kurejesha fedha mlizowapa ili kutoa chachu kwa wenzao nao kunufaika nazo. Hata vijana tunaowakabidhi pikipiki leo, watajituma kuhakikisha wanaboresha maisha yao," alisema.

Mavunde alisema serikali itaendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo katika jitihada za kuwainua wananchi kiuchumi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Benki ya CRDB, Tully Mwambapa alisema uwekezaji huo ni sehemu ya mkakati wa kitaifa wa kuwekeza katika rasilimaliwatu kama injini ya uchumi wa Tanzania.

"Huu ni uwekezaji wa makusudi katika kizazi kitakachobeba uchumi wa taifa letu. Vijana na wanawake si makundi ya kusaidiwa pekee, bali ni washirika wakuu wa ukuaji wa uchumi," alisema Tully.

Alisema tangu kuanzishwa kwa taasisi hiyo mwaka 2023, zaidi ya vijana na wanawake milioni moja wamepata mafunzo ya ujasiriamali na elimu ya fedha, huku baadhi yao wakinufaika na mitaji wezeshi zaidi ya Sh bilioni 20.4 zilizotolewa nchini kote.



Kaimu Meneja wa Hati na Vyeti Visivyo vya Mitihani wa Baraza la Mitihani Tanzania (Necta), Ndonde Mwankenja (wa tatu kushoto) akizungumza na maofisa wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) wakiongozwa na Meneja wa Huduma za Uchapishaji, Selemani Mwaitenga (wa pili kulia) wakati wa ziara ya kubadilishana uzoefu katika ofisi za baraza hilo, Dar es Salaam juzi. Kushoto kwake ni Meneja wa Nyaraka na Uchapishaji wa Mitihani wa Necta, Fabian Mbiliyeko na Mkuu wa Idara ya Ubunifu wa Michoro, Paul Masahu. (Picha na Robert Okanda).

# Mwigulu aagiza mawaziri wabaki Tanga

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Dk Mwigulu Nchemba ameagiza baadhi ya mawaziri aliofuatana nao katika ziara mkoani Tanga wabaki mkoani humo kufuatilia masuala yaliyoibuliwa na wananchi na kuyatafutia ufumbuzi.

Dk Mwigulu alitoa agizo hilo alipokuwa akizungumza na wakazi wa Soni, Bumbuli katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kituo cha Mabasi cha Soni wilayani Lushoto jana.

ya hadhara na wabunge wa Mkoa wa Tanga pamoja na wananchi kwenye sekta za ardhi, mifugo, kilimo, maji, elimu na barabara.

Awali, wakati akijibu hoja kuhusu ubovu wa barabara wilayani Lushoto, Naibu Waziri wa Ujenzi, Godfrey Kasekenya alisema Rais Samia Suluhu Hassan ametoa kibali cha kuanza ujenzi wa barabara ya njia mbili ya Soni–Bumbuli–Dindira hadi Old Korogwe.

"Barabara hii ilishatangazwa na sasa tunakamilisha taratibu za wakandarasi. Zikiwa tayari, mmoja ataanzia Soni kwa kujenga

Shemsi) kwa kujenga kilometa 9.5," alisema Kasekenya.

Alisema barabara ya sasa ya kutoka Mombo–Soni hadi Lushoto yenye urefu wa kilometa 32 imefanyiwa usanifu na inatafutiwa fedha ili ipanuliwe.

Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde alisema msajili wa hazina anamalizia uhakiki wa madeni ya zamani ya wakulima wa chai waliokuwa wanadai malipo katika Kiwanda cha Chai cha Mponde.

Silinde alisema kiwanda hicho kinachohudumia halmashauri mbili za Bumbuli na Korogwe

punguza mlundikano wa majani ya chai yaliyovunwa.

Alisema Bodi ya Chai imenunua kiwanda kingine Korogwe kinachotarajiwa kuanza kazi kabla ya Juni mwaka huu ili kupunguza mzigo unaoelekezwa katika Kiwanda cha Chai cha Mponde.

Katika hatua nyingine, Dk Mwigulu amekagua na kuzindua Shule ya Sekondari ya Amali ya Majulai iliyopo katika Kijiji cha Majulai, Kata ya Mwangoi, Tarafa ya Mlalo wilayani Lushoto.

Shule hiyo imesajiliwa, ina walimu sita na wanafunzi 89 walio-